




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



01/10/2024

## TANGAZO KWA UMMA

**DIRISHA LA UTOAJI MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,  
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU LIMEFUNGULIWA RASMI**  
**01/10/2024 HADI 20/10/2024**

**(Limetolewa kwa kuzingatia Sura ya 290 kifungu cha 37A (4)) ya Sheria ya Fedha  
ya Serikali za Mitaa)**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, anatangaza uwepo wa Tsh 700,000,000.00 kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo vikundi vyenye sifa vinatakiwa vijisajili na kuomba mkopo kuititia ofisi za Watendaji wa Vijiji zilizopo katika maeneo yenu. Vikundi vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo kabla ya kuomba mkopo:-

1. Wanakikundi wawe ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri wa miaka 18 na kuendelea isipokuwa kwa kundi la vijana ni miaka 18 hadi 45.
2. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye Ulemavu lazima kiwe kimetambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuititia Mfumo wa kielectroniki wa utoaji na Usimamizi wa mikopo.
3. Kikundi kiwe kinajishughulisha na ujasiriamali au kinakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati;
4. Kikundi cha Wanawake na Vijana lazima kiwe na wanachama kuanzia watano (5) na kuendelea, wakati kikundi cha watu Wenye Ulemavu kinatakiwa kuwa na wanachama wasiopungua wawili (2) isipokuwa pale ambapo Menejimenti ya Halmashauri imejiridhisha kuwa mlemavu amekosa mtu mwingine wa kushirikiana naye katika mradi kusudiwa anaweza kuwa mmoja (1), hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 6(1);
5. Kikundi kiwe na akaunti benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi na yenye akiba
6. Kikundi kisiwe na deni la mkopo wa Halmashauri au Taasisi yoyote ya kifedha.
7. Kikundi kisiwe na wajumbe wenye ajira rasmi.

Dr. Omary A. Nkullo  
MKUTUGENZI MTENDAJI  
KONGWA.



MKURUGENZI MIENDA  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S L P. 57  
KONGWA

**"Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi Jitokeze kushiriki Uchaguzi"**